# NAFASI YA KAMATI ZA BUNGE KATIKA UENDESHAJI WA SHUGHULI ZA BUNGE

Mhe. Pius Msekwa

[Spika wa Bunge la Tanzania]

# YALIYOMO

**Kurasa**

KAMATI ZA BUNGE ........................................................................ 1

MAJUKUMU YA KILA KAMATI ........................................................ 2

1. Kamati ya Uongozi ........................................................................ 2
2. Kamati ya Fedha na Uchumi ........................................................ 2
3. Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ........................................... 3
4. Kamati ya Hesabu za Serikali ...................................................... 4
5. Kamati ya Uwekezaji na Biashara ................................................ 4
6. Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje ................................................ 5
7. Kamati ya Kanuni za Bunge ......................................................... 6
8. Kamati ya Ulinzi na Usalama ....................................................... 6
9. Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ........................ 7
10. Kamati ya Huduma za Jamii ....................................................... 7
11. Kamati ya Maliasili na Mazingira ............................................... 8
12. Kamati ya Maendeleo ya Jamii ................................................... 9
13. Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa ...................................... 10
14. Kamati ya Kilimo na Ardhi ......................................................... 10
15. Kamati ya Miundombinu ............................................................. 11

UTEUZI WA WAJUMBE WA KAMATI ZA KUDUMU ZA BUNGE ........................................................................ 12

Nafasi ya Kamati za Kudumu za Bunge katika Shughuli za Bunge ... 13

MAPENDEKEZO YA "MABUNGE YA JUMUIYA YA MADOLA" KUHUSU UIMARISHAJI WA KAMATI ZA BUNGE ........ 14
1. PENDEKEZO ........ 15
2. PENDEKEZO ........ 16
3. PENDEKEZO ........ 17
4. PENDEKEZO ........ 17
5. PENDEKEZO ........ 18
6. PENDEKEZO ........ 18
7. PENDEKEZO ........ 19
8. PENDEKEZO ........ 19
9. PENDEKEZO ........ 20
KAMATI ZA BUNGE ZIMA ........ 20

# KAMATI ZA BUNGE

Kuna aina mbili kubwa za Kamati za Bunge, kila aina ikiwa na majukumu yake maalum. Aina hizo ni:

(a) Kamati za Kudumu za Bunge, na
(b) Kamati za Bunge Zima.

Uendeshaji wa shughuli zote za Bunge huanzia kwenye Kamati zake za Kudumu, kwa ajili ya uchambuzi wa shughuli hizo kabla hazijawasilishwa kwenye Bunge lenyewe. Kwa ajili hiyo, Bunge limejiundia Kamati za Kudumu zifuatazo:-

(a) Kamati ya Uongozi;
(b) Kamati ya Fedha na Uchumi;
(c) Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala;
(d) Kamati ya Hesabu za Serikali;
(e) Kamati ya Uwekezaji na Biashara;
(f) Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje;
(g) Kamati ya Kanuni za Bunge;
(h) Kamati ya Ulinzi na Usalama;
(i) Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge;
(j) Kamati ya Huduma za Jamii;
(k) Kamati ya Maliasili na Mazingira;
(l) Kamati ya Maendeleo ya Jamii;
(m) Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa;
(n) Kamati ya Kilimo na Ardhi;

(o) Kamati ya Miundombinu.

## MAJUKUMU YA KILA KAMATI

Kila moja ya Kamati zilizoorodheshwa hapo juu imepangiwa majukumu yake na Kanuni za Bunge kama ifuatavyo:-

### 1. Kamati ya Uongozi

Kumshauri Spika kuhusu jambo lolote linalohusu uendeshaji wa shughuli za Bunge, hususan kuhusu ratiba ya jumla ya shughuli za Bunge kwa kila mkutano wake.

### 2. Kamati ya Fedha na Uchumi

a) Inasimamia Wizara zifuatazo:

- Wizara ya Fedha;
- Ofisi ya Rais (Mipango na Ubinafsishaji);

b) Majukumu yake ni haya yafuatayo:

(i) Kushughulikia Bajeti za Wizara hizo.

(ii) Kushughulikia mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya kila mwaka.

(iii) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inay-

opendekezwa kuridhiwa na Bunge ambayo chanzo chake ni Wizara hizo.

(iv) Kushughulikia taarifa za kila mwaka za utendaji na hesabu zilizokaguliwa na Mashirika ya Umma yaliyoko chini ya Wizara hizo.

(v) Kufuatilia utekelezaji unaofanywa na Wizara hizo kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(b) ya Katiba.

## 3. Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala

a) Inasimamia Wizara zifuatazo:

- Ofisi ya Rais (TAMISEMI, Utumishi na Utawala Bora);
- Ofisi ya Waziri Mkuu;
- Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba;

b) Majukumu yake ni haya yafuatayo:

(i) Kushughulikia Bajeti za Wizara hizo.

(ii) Kushughulikia Miswada ya Sheria, na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge, ambayo chanzo chake ni Wizara hizo.

(iii) Kushughulikia taarifa za kila mwaka za utendaji na hesabu zilizokaguliwa na Mashirika ya Umma yaliyo

chini ya Wizara hizo.

(iv) Kufuatilia utekelezaji unaofanywa na Wizara hizo, kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(b) ya Katiba.

4. **Kamati ya Hesabu za Serikali**

Majukumu yake ni haya yafuatayo:

(i) Kushughulikia maeneo yenye matatizo sugu yaliyoainishwa katika Taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali kuhusu Serikali Kuu.

(ii) Kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yaliyokwisha kutolewa na Kamati hiyo ya kuondoa matatizo husika, ili yasionekane tena katika taarifa zitakazofuata.

5. **Kamati ya Uwekezaji na Biashara**

(a) Itasimamia Wizara zifuatazo:

- Wizara ya Viwanda na Biashara;
- Wizara ya Nishati na Madini;
- Wizara ya Ushirika na Masoko;

(b) Majukumu yake ni haya yatuatayo:

(i) Kushughulikia Bajeti za Wizara hizo.

(ii) Kushughulikia Miswada ya Sheria, na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge ambayo chanzo chake ni Wizara hizo.

(iii) Kushughulikia taarifa za kila mwaka za utendaji na hesabu zilizokaguliwa za Mashirika ya Umma yaliyo chini ya Wizara hizo.

(iv) Kushughulikia utekelezaji unaofanywa na Wizara hizo kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(b) ya Katiba.

6. **Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje**

Majukumu yake ni haya yafuatayo:-

(i) Kushughulikia Bajeti ya Wizara hiyo.

(ii) Kushughulikia Miswada ya Sheria, na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge, ambayo chanzo chake ni Wizara hiyo.

(iii) Kushughulikia taarifa za utendaji wa hesabu zilizokaguliwa za Mashirika ya Umma yaliyo chini ya Wizara hiyo.

(iv) Kufuatilia utekelezaji unaofanywa na Wizara hiyo kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(b) ya Katiba.

## 7. Kamati ya Kanuni za Bunge

Majukumu yake ni haya yafuatayo:-

(i) Kufikiria na kutoa mapendekezo juu ya kufanya mabadiliko katika Kanuni za Bunge.

(ii) Kuchunguza na kutoa taarifa juu ya pendekezo lolote linalohusu Kanuni za Bunge ambalo limepelekwa kwa Kamati hiyo na Spika au Mbunge yeyote.

(iii) Kuchunguza na kutoa taarifa juu ya lalamiko lolote kuhusu uamuzi wa Spika ambalo limepelekwa kwake na Mbunge yeyote.

## 8. Kamati ya Ulinzi na Usalama

(a) Itasimamia shughuli za Wizara zifuatazo:

- Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa;
- Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi;

(b) Majukumu yake ni haya yafuatayo:-

(i) Kushughulikia Bajeti za Wizara hizo.

(ii) Kushughulikia Miswada ya Sheria, na Mikataba inay-

opendekezwa kuridhiwa na Bunge, ambayo chanzo chake ni Wizara hizo.

(iii) Kushughulikia taarifa za kila mwaka za utendaji na hesabu zilizokaguliwa za Mashirika ya Umma yaliyo chini ya Wizara hizo.

(iv) Kufuatilia utekelezaji unaofanywa na Wizara hizo kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(b) ya Katiba.

## 9. Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge

Majukumu yake ni haya yafuatayo:-

(i) Kuchunguza masuala yote yahusuyo Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge yanayopelekwa kwake na Spika.

(ii) Kushughulikia mambo yanayohusu maadili ya Wabunge.

(iii) Kufikiria jambo lingine lolote litakalopelekwa kwake na Spika.

## 10. Kamati ya Huduma za Jamii

(a) Itasimamia shughuli za Wizara zifuatazo:-

- Wizara ya Afya.
- Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu.

- Wizara ya Elimu na Utamaduni.

(b) Majukumu yake ni haya yafuatayo:-

(i) Kushughulikia Bajeti za Wizara hizo.

(ii) Kushughulikia Miswada ya Sheria, na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge, ambayo chanzo chake ni Wizara hizo.

(iii) Kushughulikia taarifa za kila mwaka za utendaji na hesabu zilizokaguliwa na Mashirika ya Umma yaliyo chini ya Wizara hizo.

(iv) Kufuatilia utekelezaji unaofanywa na Wizara hizo kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(b) ya Katiba.

11. **Kamati ya Maliasili na Mazingira**

(a) Itasimamia shughuli za Wizara zifuatazo:-

- Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira na Kuondoa Umaskini)
- Wizara ya Maliasili na Utalii.

(b) Majukumu yake ni haya yafuatayo:-

(i) Kushughulikia Bajeti za Wizara hizo.

(i) Kushughulikia Miswada ya Sheria, na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge, ambayo chanzo chake ni Wizara hizo.

(ii) Kushughulikia taarifa za kila mwaka za utendaji na hesabu zilizokaguliwa za Mashirika ya Umma yaliyo chini ya Wizara hizo.

(iii) Kufuatilia utekelezaji unaofanywa na Wizara hizo kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(b) ya Katiba.

12. **Kamati ya Maendeleo ya Jamii**

(a) Itasimamia shughuli za Wizara zifuatazo:-

- Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto.
- Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo.

(b) Majukumu yake ni haya yafuatayo:-

(i) Kushughulikia Bajeti za Wizara hizo.

(ii) Kushughulikia Miswada ya Sheria, na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge, ambayo chanzo chake ni Wizara hizo.

(iii) Kushughulikia taarifa za kila mwaka za utekelezaji na hesabu zilizokaguliwa za Mashirika ya Umma yaliyo

chini ya Wizara hizo.

(iv) Kufuatilia utekelezaji unaofanywa na Wizara hizo kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(b).

## 13. Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa

Majukumu yake ni haya yafuatayo:-

(i) Kushughulikia maeneo yenye matatizo sugu yaliyoainishwa katika Taarifa ya Mdhibiti Mkuu wa Serikali kuhusu Serikali za Mitaa.

(ii) Kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yaliyokwisha kutolewa na Kamati hiyo ya kuondoa matatizo husika ili yasionekane tena katika taarifa zitakazofuata.

## 14. Kamati ya Kilimo na Ardhi

(a) Itasimamia shughuli za Wizara zifuatazo:-

- Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi.
- Wizara ya Kilimo na Chakula.
- Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo.

(b) Majukumu yake ni haya yafuatayo:-

(i) Kushughulikia Bajeti za Wizara hizo.

(ii) Kushughulikia Miswada ya Sheria, na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge, ambayo chanzo chake ni Wizara hizo.

(iii) Kushughulikia taarifa za kila mwaka za utendaji na hesabu zilizokaguliwa za Mashirika ya Umma yaliyo chini ya Wizara hizo.

(iv) Kufuatilia utekelezaji unaofanywa na Wizara hizo kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(b) ya Katiba.

15. **Kamati ya Miundombinu**

(a) Itasimamia shughuli za Wizara zifuatazo:-

- Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi
- Wizara ya Ujenzi

(b) Majukumu yake ni haya yafuatayo:-

(i) Kushughulikia Bajeti za Wizara hizo.

(ii) Kushughulikia Miswada ya Sheria, na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge, ambayo chanzo chake ni Wizara hizo.

(iii) Kushughulikia taarifa za kila mwaka za utendaji na hesabu zilizokaguliwa za Mashirika ya Umma yaliyo chini ya Wizara hizo.

(iv) Kufuatilia utekelezaji unaofanywa na Wizara hizo kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(b) ya Katiba.

## UTEUZI WA WAJUMBE WA KAMATI ZA KUDUMU ZA BUNGE

Wajumbe wa kila Kamati ya Kudumu ya Bunge huteuliwa na Spika, ambaye katika kufanya uteuzi huo, anawajibika kuzingatia misingi ifuatayo:-

a) Atazingatia aina za Wabunge na kuwagawa Wabunge wa kila aina kwa kila Kamati. Isipokuwa kwamba Mawaziri na Naibu Mawaziri hawateuliwi kuwa wajumbe wa muda wote katika kamati yoyote. Lakini kwa kuwa ni wajumbe wa Kamati inayoshughulikia jambo fulani la Wizara hiyo wakati ule ambapo Kamati husika inashughulikia jambo hilo tu.

b) Kwa kadri inavyowezekana, atazingatia matakwa ya Wabunge wenyewe, yaani wangependelea kupangwa kwenye Kamati gani.

c) Atazingatia haja kwa kila Kamati ya kuwa na Wabunge wenye uzoefu na ujuzi maalum (kama wapo) kuhusu kazi za kamati hiyo.

## Nafasi ya Kamati za Kudumu za Bunge katika Shughuli za Bunge

Kamati za Kudumu za Bunge ndizo hasa zenye nafasi nzuri ya kusimamia utekelezaji unaofanywa na Serikali kuliko Bunge lenyewe, kwa sababu kubwa tatu zifuatazo:-

(a) Kamati za Bunge zina wajumbe wachache, ambao kwa hiyo wanayo fursa kubwa ya kuchambua kwa undani shughuli zote zinazowasilishwa na Serikali, kuliko Bunge lenyewe ambalo lina idadi kubwa ya Wabunge.

(b) Katika mijadala ya Kamati za Bunge hakuna wasikilizaji, Waandishi wa habari, wala vipaza sauti vya kutangaza nje ya ukumbi maneno yanayosemwa ndani ya vikao vya Kamati. Kwa maneno mengine, vikao vya Kamati za Bunge ni vya faragha, kwa hiyo hakuna nafasi ya malumbano ya kisiasa katika vikao hivyo.

(c) Katika vikao vyote vya Kamati za Bunge, Mawaziri wanaruhusiwa kufuatana na Wataalam wa Wizara zao, na wataalam hao wanaruhusiwa kuchangia kwa kutoa maelezo na ufafanuzi wowote unaohitajika katika mambo ya utekelezaji yanayohusu wizara zao. Hivyo ni nafasi nzuri kwa Wabunge kuelewa kwa undani zaidi mipango na mikakati ya utekelezaji iliyopo, ili kuwawezesha kuhoji mipango hiyo na kutoa ushauri unaofaa.

Kwa mujibu wa Ibara ya 63(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano,

Bunge ndicho chombo chenye madaraka, kwa niaba ya wananchi, ya kusimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano pamoja na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake.

Kwa sababu nzuri hizo zilizoelezwa katika fasili za (a) hadi (c) hapo juu, kazi hiyo ya kuisimamia na kuishauri Serikali inafanywa kwa ufanisi zaidi katika Kamati kuliko katika Bunge lenyewe.

## MAPENDEKEZO YA "MABUNGE YA JUMUIYA YA MADOLA" KUHUSU UIMARISHAJI WA KAMATI ZA BUNGE

Mnamo mwaka 1995, Chama cha Wabunge wa Commonwealth kiliunda timu yake ya kufanya utafiti (study Group) na kutoa mapendekezo ya jinsi gani Kamati za mabunge ya nchi za Jumuiya ya Madola zingeweza kuimarishwa ili kuwezesha mabunge hayo kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi. Taarifa ya Timu hiyo ilitolewa mjini London mwishoni mwa mwaka 1999 ikiwa na kichwa cha habari kifuatacho ***Parliamentary Committees: Enhancing Democratic Governance.***

Katika Taarifa hiyo yalitolewa mapendekezo mengi ya jinsi ya kuimarisha Kamati za Mabunge hayo. Lakini kwanza ilitoa maelezo kuhusu ukuaji wa mfumo wa Kamati katika mabunge hayo kwamba umetokana na hali halisi ya ukuaji wa majukumu ya mabunge yenyewe, kama ifuatavyo:-

> "The Committee System in Commonwealth Parliaments has, for the most part, developed in response to the need to relieve the pressure of business on the floor of the House; or in response to new obligations or to demands for the House to perform new functions involving detailed investigation which are unsuited to a large assembly."

Baada ya kutamka hivyo, Taarifa hiyo baadaye inatoa mapendekezo kadhaa katika sura yake ya kumi ya kuimarisha muundo pamoja na utendaji kazi za Kamati za Bunge.

Bunge letu limeyafanyia tathmini mapendekezo hayo, na matokeo ya tathmini hiyo ni kwamba asilimia 99 (99%) ya mapendekezo yote yamekwisha kutekelezwa kwa ukamilifu kabisa kwa upande wetu. Takwimu hiyo ilichapishwa katika jarida linaloitwa ***The Parliamentarian: Journal of the parliaments of the Commonwealth*** Toleo la Nne 2003 Uk. 361 – 365.

Mapendekezo muhimu yaliyomo, pamoja na tathmini ya utekelezaji wake kwa upande wetu, ni kama ifuatavyo:

1. **PENDEKEZO**

   Kwamba uteuzi wa wajumbe wa Kamati za Bunge utegemee zaidi uzoefu na ujuzi wao, ili Wabunge wenye ujuzi maalum waweze kutumia ujuzi wao huo katika kuongeza ufanisi wa kazi wa Kamati husika.

**TATHMINI**:

Hivyo ndivyo inavyofanyika katika Bunge letu, kwani Kanuni ya 87(2)(d) ya Kanuni za Bunge la Tanzania inaelekeza kwamba Spika anapoteua na kuwapanga Wabunge katika Kamati mbalimbali za Bunge, "atazingatia hoja kwa kila Kamati kuwa na Wabunge wenye uzoefu au ujuzi maalum kuhusu kazi za Kamati hiyo."

Kwa hiyo, kwa mfano, Wabunge wenye ujuzi wa uchumi hupangwa kwenye Kamati za kiuchumi, n.k.

Na kwa kuwa fasili ya (c) ya Kanuni hiyo hiyo ya 87 inamwelekeza Spika "kwa kadri inavyowezekana, azingatie matakwa ya Wabunge wenyewe," Spika huwa anawaomba Wabunge wajaze fomu maalum ya kuonyesha wangependelea wapangwe katika Kamati gani. Hii inamrahisishia kazi ya kuwapanga siyo tu katika Kamati ile ambayo wana ujuzi wa shughuli zake, bali pia wao wenyewe wanapenda kuwa katika Kamati hiyo.

2. **PENDEKEZO**

Ili kujenga uzoefu wa kutosha wa kazi za kila Kamati kwa wajumbe wake, ingefaa wajumbe wa kila Kamati waitumikie Kamati hiyo kwa kipindi chote cha miaka mitano ya maisha ya Bunge"

**TATHMINI**

Katika siku za nyuma Bunge letu limekuwa na utaratibu wa kubadilisha Wajumbe na kuwapanga katika Kamati tofauti kila mwaka, lakini tayari tumekwisha kufikia hatua ya kuwabadilisha mara moja tu

baada ya miaka miwili na nusu. Hatua itakayofuata katika Bunge la 2005 – 2010 ni kuwaacha Wabunge katika Kamati zao kwa kipindi chote cha miaka mitano ili wajenge uzoefu wa kutosha wa kazi za Kamati zao.

3. **PENDEKEZO**

Kwa mantiki hiyo hiyo ya kujenga uzoefu, wajumbe wa Kamati wasiwe wanabadilishwa ghafla kwa kuweka wajumbe wapya wasiokuwa na uzoefu na kazi za Kamati husika.

**TATHMINI**

Kutokana na wazo la kuwaacha wajumbe wa kila kamati waendelee kutumikia amati zao kwa kipindi chote cha miaka mitano ya maisha ya Bunge, tatizo hili halipo kabisa katika Bunge letu. Wajumbe wapya hupangwa katika kamati baada tu ya uchaguzi mdogo, ambao unaingiza Mbunge mpya ambaye hakuwa amepangwa katika kamati yoyote.

4. **PENDEKEZO**

Inafaa idadi ya wajumbe wa kila kamati iwe ndogo, ili kuleta ufanisi zaidi katika utendaji kazi wake.

**TATHMINI**

Wajumbe wa kila Kamati katika Bunge letu hawazidi thelathini. Hiyo ni idadi muafaka kabisa kuwezesha Kamati kuendesha shughuli zake kwa ufanisi.

5. **PENDEKEZO**

Kwamba katika vikao vya Kamati za Bunge, wajumbe wawe huru kutoa mawazo yao kama wanavyoona inafaa, bila kubanwa na msimamo ya vyama vyao.

**TATHMINI**

Katika Kamati za Bunge letu, wajumbe wa vyama mbali mbali wanafanya kazi kwa ushirikiano na kwa kuzingatia maslahi ya Taifa tu. Hawabanwi na misimamo ya Vyama vyao vya Siasa. Hali hii pia inasaidia na utaratibu uliopo kwamba katika vikao vya Kamati za Bunge vyombo vya habari haviruhusiwi kuhudhuria. Hiyo inawapa wajumbe wa Kamati kutoa mawazo yao kama wanavyoona inafaa, bila kuhofia kwamba vyombo vya habari vinaweza kuyapotosha.

6. **PENDEKEZO**

Ni muhimu kwa Kamati za Bunge kupewa nyenzo za kutosha za kufanyia kazi, kwa maana ya maafisa wa kuzifanyia utafiti, pamoja na fedha za kutosha ili kuziwezesha Kamati hizo kufanya kazi zake kwa ufanisi.

**TATHMINI**

Kamati za Bunge letu hupangiwa na Spika ratiba ya kutekeleza kazi zake, ambazo ni kushughulikia mambo yale yote yaliyopangwa kuwasilishwa Bungeni katika mkutano unaofuata. Ratiba hiyo inatenga siku za kutosha kuweza kushughulikia mambo hayo na fedha za kutosha kutekeleza ratiba hiyo kutolewa katika bajeti ya Bunge. Isipokuwa kwamba inapotokea kuwa Kamati inajipangia

kutembelea baadhi ya miradi ili kukagua utekelezaji wake, bajeti ya Bunge huwa haina uwezo wa kulipia gharama za ziara kama hizo, lakini Wizara zinazohusika mara nyingi hulipia gharama za ziara hizo za wajumbe wa Kamati husika.

Kwa upande wa Kamati kupatiwa Maafisa Utafiti, bado kuna upungufu mkubwa katika utekelezaji wa suala hilo. Lakini ikizingatiwa kwamba Kamati zetu kwa kawaida zinashughulikia mambo yale tu yanayoletwa kwake na Serikali, kama inavyoonyeshwa katika orodha ya majukumu ya kila Kamati; na kwa kuwa mambo hayo tayari yanakuwa yamekwisha kufanyiwa utafiti na Serikali kabla ya kuyaleta kwenye Kamati, Kamati yenyewe inakuwa haina tena sababu ya msingi ya kufanya utafiti mpya juu ya mambo yale yale.

7. **PENDEKEZO**

Muundo wa Kamati za Bunge ingefaa uwe unaziwezesha kamati hizo kusimamia Wizara za Serikali, yani kila Kamati ikiwa na Wizara zake mahsusi.

**TATHMINI**

Hivyo ndivyo ulivyo muundo wa Kamati za Bunge la Tanzania, kama inavyoonyeshwa hapo juu katika sehemu inayoeleza majukumu ya Kamati hizi.

8. Kwamba ingefaa miswada ya Sheria ipelekwe kwenye Kamati inayohusika kabla ya kusomwa mara ya pili.

**TATHMINI**

Hivyo ndivyo inavyofanyika katika Bunge letu. Spika hupeleka kila muswada kwenye Kamati inayohusika hata kabla haujawasilishwa Bungeni kusomwa mara ya kwanza, ili iweze kufikiriwa na Kamati zinazopelekewa miswada hiyo katika kipindi cha wiki mbili ambacho hutengwa kwa ajili ya kazi za Kamati kabla ya kila mkutano wowote wa Bunge.

9. **PENDEKEZO**

Kwamba ingefaa Uwenyekiti wa Kamati mbali mbali ugawanywe baina ya wabunge wa Chama Tawala na Wabunge wa Vyama vya Upinzani.

**TATHMINI**

Kutokana na uchache wa Wabunge wa vyama vya upinzani ulivyokuwa katika Bunge la 1995 hadi 2000; na uchache mkubwa zaidi uliojitokeza katika Bunge la 2000 hadi 2005, pendekezo hili lisingeweza kutekelezwa. Lakini pamoja na hali hiyo, utaratibu wetu ni kwamba kila kamati inachagua Mwenyekiti wake. Wenyeviti wa Kamati hawateuliwi na Spika. Kwa hiyo Kamati inayopenda kuchagua Mwenyekiti wake kutoka Kambi ya Upinzani inao uhuru kamili wa kufanya hivyo. Hakuna kizuizi chochote kinachowazuia wasifanye hivyo.

## KAMATI ZA BUNGE ZIMA

Kamati za Bunge zima vile vile zipo za aina mbili. Aina ya kwanza ni Kamati ya Bunge zima inayoundwa kwa madhumuni ya kupitia vifungu

kimoja kimoja vya miswada ya sheria katika mchakato wa kuifikiria miswada hiyo Bungeni.

Baada ya muswada wowote wa Sheria kuwa umesomwa mara ya pili kulingana na taratibu zilivyo za kushughulikia miswada ya Sheria, Bunge hujigeuza kuwa Kamati ya Bunge zima, kwa lengo la kufikiria na kupitisha kifungu kimoja kimoja cha muswada unaohusika. Taratibu zote zinazohusu uendeshaji wa shughuli za Bunge zinatumika pia katika Kamati ya Bunge Zima, isipokuwa kuna tofauti mbili zifuatazo:-

(a) hoja inayotolewa katika Kamati ya Bunge zima haihitaji kuungwa mkono, na

(b) kwa idhini ya Mwenyekiti wa Kamati, mjumbe yeyote aweza kupewa nafasi ya kuzungumza mara mbili juu ya suala moja.

Aina ya pili ya Kamati ya Bunge zima ni ile inayoundwa kwa madhumuni ya kufikiria na kupitisha vifungu kimoja kimoja cha makadirio ya matumizi ya kila Wizara wakati wa Mkutano wa bajeti. Aina hii ya Kamati ya Bunge zima inaitwa **Kamati ya Matumizi,** kwa sababu kazi yake ni kufikiria makadirio ya matumizi ya Wizara inayohusika.

Bunge hujigeuza kuwa Kamati ya Matumizi mara baada ya Waziri aliyewasilisha hoja ya kuomba Bunge lipitishe makadirio ya Wizara yake, kuhitimisha hoja yake hiyo kwa kutoa ufafanuzi wa baadhi ya mambo yaliyoelezwa na Wabunge wakati wakichangia mawazo yao (ama kwa

kuzungumza au kwa maandishi) katika hoja ya Waziri huyo.

Taratibu za uendeshaji wa shughuli katika Kamati ya Matumizi ni sawa na zile zilizoelezwa kwa upande wa Kamati ya Bunge zima inayoshughulikia miswada ya Sheria.